# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## KIKAO CHA AROBAINI NA SITA

**12 JUNI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### KIKAO CHA AROBAINI NA SITA – TAREHE 12 JUNI, 2023

## I. DUA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**580. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itashughulikia suala la kuboresha ujira wa Madereva wa magari ya IT.

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**581. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali isiongeze kundi la Wanaume kwa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri.

**582. MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kutengeneza barabara zote mbovu katika Mkoa wa Simiyu.

**583. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi katika maeneo ya Vijijini.

**584. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma ya kifungua kinywa kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi.

**585. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi za kisasa za Walimu katika kila Shule nchini.

**586. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatunga Sera ya Ugatuaji wa Madaraka na kutunga Sheria ili kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mtaa.

**587. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Uyui - Tabora katika Kata ya Tura na Wilaya ya Ikungi - Singida.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**588. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali imejiimarisha vipi kukagua miamala ya uhamishaji bei ya mauziano ya bidhaa/huduma za Makampuni ya Kimataifa.

**WIZARA YA AFYA:**

**589. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itapeleka vifaa kwenye Jengo Jipya la Mama na Mtoto katika Hospitali ya META Mkoani Mbeya.

**590. MHESHIMIWA ESTER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mchango gani katika kuboresha huduma za Hospitali ya KCMC ambayo inatoa huduma za afya kwa Kanda ya Kaskazini.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**591. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati mkubwa wa Barabara Kuu ya Makambako - Njombe.

**592. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Meli tatu kwa ajili ya Ziwa Tanganyika kama ilivyoahidi.

**593. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaboresha Kivuko cha Kinesi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**594. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani kuboresha utendaji wa Shirika la Mbolea (TFC) ili kusambaza pembejeo kwa Wakulima kwa wakati.

**WIZARA YA MAJI:**

**595. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza Bonde la Mto Ruvu kwa kushirikiana na Wananchi.

**596. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mkandarasi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Vijiji 33 vya Jimbo la Bunda ataanza kazi.

**597. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itachimba Visima katika Shule ya Sekondari Ndono Uyui.

## WIZARA YA NISHATI:

**598. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini tatizo la kukatika umeme mara kwa mara Mkoani Lindi litakwisha.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**599. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itafanya tathmini ya Kampuni zilizo chini ya NARCO ili kuona tija zake katika uchumi.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**600. MHESHIMIWA JUSTINE LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Minara ya Simu katika Kata za Masisiwe, Udwekwa na Nyanzwa Wilayani Kilolo.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**12 JUNI, 2023** **KATIBU WA BUNGE**